JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:

TAARIFA YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 30 JUNI 2009

(Imeandaliwa kwa kuzingatia Kanuni ya 120 na kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007)

Taarifa imechapishwa na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge
OFISI YA BUNGE
DODOMA

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Pamoja na masuala mengine,naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu tukufu. Vile vile Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge. Mimi pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati yetu tunakuahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Bunge, Kanuni za Bunge, mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adimu kuwapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwa wabunge na zaidi nikushukuru wewe mheshimiwa spika kwa kutuchagua kuwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika,Taarifa hii ya kamati inatoa uchambuzi wa kina, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma juu ya Hesabu, ufanisi wa Mashirika ya Umma na utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsishaji nchini. Maoni

na Mapendekezo haya ni kufuatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Mashirika ya Umma nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni,2009.

1.1. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati yameainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007 chini ya Kanuni ya 115 kifungu cha 13 katika Fasili Ndogo (a) hadi (e). Majukumu hayo ya Kamati ni kama ifuatavyo:

a) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2009 jumla ya Mashirika ya Umma 156 yaliwasilisha Taarifa za hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ambapo taarifa za Mashirika 51 hii ikiwa ni sawa na 32.6 % ya taarifa zote zilizowasilishwa zilikaguliwa na kukamilika, Taarifa 105 zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi ambazo ni sawa na 67.4%ya taairifa zote zilizowasilishwa. Aidha Mashirika 10 hayakuwasilisha taarifa zao za hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili zikaguliwe kama sheria inavyoelekeza.

Mashirika ambayo hayakuwasilisha hesabu zao kwa ukaguzi ni

pamoja na

- Bodi ya Kahawa Tanzania,
- Chuo Kikuu cha Dodoma,
- General Tyre East Africa Limited,
- Kilimanjaro Airport Development Company,
- CARMATEC,
- Baraza la kiswahili la Taifa,
- Taasisi ya Chakula na Lishe na
- Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).

Kamati imemtaka Msajili wa Hazina alete taarifa rasmi kwa Bunge ni kwa nini Mashirika haya hayakuwasilisha taarifa zao kwa ukaguzi na hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi ya Watendaji na Bodi za Wakurugenzi kwa kukiuka Sheria ya Mashirika ya Umma na Sheria ya Ukaguzi ya Taifa. Kwa upande wa Kampuni ya General Tyre East Africa Limited, Kamati itatoa maelezo yake rasmi hapa chini. Kampuni ya KADCO inahitaji uchunguzi maalumu na utashughulikiwa katika shughuli za Kamati zijazo.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kamati, Taarifa za Mashirika 78 kati ya taarifa za mashirika 105 zilizokaguliwa zimejadiliwa kikamilifu. Hii ni sawa na 74.2% ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

b) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika taarifa za kila mwaka za Mashirika hayo na kutoa mapendekezo na ushauri wa namna ya kuyaondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wa Kamati, imebainika kuwa maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za umma yanahusisha ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake na kuchelewa kurejesha marejesho ya masurufu (kwa mfano katika Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN) hadi juni 30, 2008 milioni 146 zilikuwa hazijarejeshwa).

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limekuwa ni tatizo kubwa katika Mashirika mengi ya umma ni kutokuwepo miongozo toka kwa msajili wa hazina itakayosaidia Mashirika kufuata sheria na taratibu ama miongozo hiyo kutozingatiwa na Wizara mama au Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ya Mashirika.

Aidha uzoefu umeonyesha kuwa kutowajibika ipasavyo kwa bodi za mashirika Kunaathiri ufanisi wa mashirika kutowajibika huko kunachangiwa na ukosefu wa ubunifu katika Menejimenti nyingi za Mashirika ikiwemo kutofikiria namna bora ya kuongeza tija katika kipindi hiki na sio kutoa huduma tu.

Mheshimiwa Spika,usimamizi wa mikataba (contract management) limeendelea kuwa tatizo kubwa na limeleta hasara kwenye mashirika mengi ya umma,mikataba mingi imeingiwa kwa gharama kubwa na masharti yake ni magumu

kiutekelezaji hali inayosababisha mashirika kupata hasara kutokana na utekelezaji wa mikataba hiyo. Baadhi ya mikataba iliyobainika kuwa na kasoro ni pamoja na ule wa matangazo ya hifadhi za Taifa kupitia TTB na cable news net work ulioigharimu TANAPA shilingi 246 milioni.

Mheshimiwa spika,tatizo lingine ni Serikali kutoa udhamini (guarantee) kwa mikopo ambayo ni vigumu kulipika na hivyo kuleta hasara kubwa kwa Mashirika ya Umma, Miongoni mwa mikopo hiyo ni ile inayotolewa kwa makampuni binafsi na ile ambayo Serikali inakopa hususan kutoka kwenye Mifuko ya Pensheni.

Mheshimiwa spika,hadi kufikia Juni 30, 2008 Serikali ilikuwa imetoa udhamini wa jumla ya shilingi bilioni 367,362,994,845.41 kwenye Mashirika ya umma na hadi kufikia Juni 30, 2009 udhamini wa serikali kwenye mikopo hiyo uliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 410,111,988,412.86 hali inayodhihirisha umuhimu wa serikali kutoendelea kutoa dhamana kwa mikopo ambayo hailipiki.

c) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Kamati hiyo ili kuondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati kwa Mwaka 2009/2010 na Majibu ya Serikali juu ya hoja za Kamati vilipata nafasi ya kujadiliwa hapa Bungeni baada ya kuwasilishwa tarehe 21 Aprili, 2010. Hata hivyo, kwa lengo la kufuatilia utekelezwaji wa

mapendekezo yanayotolewa na Kamati, Kamati yetu imeendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake kila mara. Tunatarajia kuwa na kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Serikali italeta majibu ya hoja za Kamati mbele ya Bunge lako tukufu ili kukamilisha 'Accountability loop'.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Kamati kwa Mwaka 2008/2009, hoja zifuatazo ziliibuliwa na Kamati ili kuweza kupata ufafanuzi wa kutosha toka Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Mashirika ya umma

1. Suala la Kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa huru kiutendaji na kuipa rasilimali za kutosha sambamba na kurekebisha Sheria ya uanzishwaji wa Ofisi hiyo(CAP 418) ili kuipa uwezo wa kuyasimamia Mashirika ya Umma ipasavyo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Mashirika ya Umma Nchini, hadi hivi sasa jambo hili halijatekelezwa kikamilifu. Licha ya marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina yaliyofanyika katika Bunge la Tisa, bado Sheria haikidhi haja ya kuwa na Ofisi inayosimamia ipasavyo Mashirika ya Umma (Office of Public Entreprises –OPE). Hali hii inakwaza utendaji na ufanisi wa Mashirika na hatimaye Serikali kujikuta inabeba mzigo mkubwa wa kuendesha Mashirika ambayo kimsingi inapaswa yajiendeshe.
2. Orodha ya Mashirika na Makampuni ambayo Serikali imewekeza mitaji bado haijatolewa na kumekuwapo na tofauti ya taarifa ya idadi ya mashirika yaliyopo kwenye

orodha ya msajili wa Hazina na ile ya ofisi ya Taifa ya ukaguzi, taarifa hii ni muhimu katika kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa malengoyaliyokusudiwa. Miongoni mwa mashirika ambayo Serikali ina hisa lakini lakini vyeti vya hisa havijawasilishwa ni pamoja na; Aitel Tanzania iliyojulikana kama celtel na zain hapo awali, Mbeya Cement Company, BP Tanzania na National Bank of Commarce.

3. Serikali ijiepushe na kuingilia mipango kazi ya Mashirika ya umma hasa kuagiza utoaji wa fedha kwaajili ya malipo mbali mbali ambayo hayakupangiwa bajeti na mashirika husika, Mfano katika jambo hili ni deni la shilingi bilioni 53 ambazo Bodi ya mikopo ilikopa kwa udhamini wa Serikali toka kwenye mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa umma (PSPF) deni ambalo halijalipwa na linaendelea kukua kutokana na riba. Kamati imeitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu mkopo huu na namna ambavyo utalipwa ili kuhakikisha kuwa mfuko wa PSPF unaendelea kutoa huduma zake.

4. Kamati ilipendekeza kwa Serikali juu ya uanzishaji wa Special Investment Fund kama ilivyokuwa imependekezwa hapo awali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili fedha za ziada zinazotolewa na mashirika ya umma ziwekwe kwenye mfuko huo kwa madhumuni ya uwekezaji na upatikanaji wa mitaji. Tanzania Public Investments Fund utakuwa ni kama Sovereign Wealth Fund na utawekeza kwenye

Mashirika ya Umma yenye kuhitaji Mitaji na baada ya Mashirika kuanza kupata Faida kuuza Hisa katika Soko la Hisa na kurejesha Fedha. Mfuko utokane na Makato ya asilimia 10 ya Mapato ya Mashirika ya Umma yenye kupata Faida. Mfuko huu utaondoa mzigo kwa Serikali kutoa mitaji kwa Mashirika kila wakati. Serikali inapaswa kutoa jibu kuhusu hoja hii.

5. Pendekezo la Wabunge kutokuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya umma bado halijatekelezwa na Mawaziri bado wanateua Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Pendekezo hili limetolewa na Kamati kwa miaka mitatu mfululizo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameendelea kulitolea mapendekezo. Kamati itaandaa orodha ya Wabunge wote walio kwenye Bodi za Mashirika ya Umma na inashauri waondolewe ili wabunge wabaki na Kazi ya Kuisimamia Serikali (oversight role). Kitendo cha Mawaziri kuendelea kuteua Wabunge kwenye Bodi za Mashirika ya Umma ni dharau kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bunge lako Tukufu.

6. Ilipendekezwa kuwa Shirika la maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ligawanywe ili kupata Mashirika mawili ya Umma moja likisimamia utoaji wa leseni na Udhibiti wa Uchimbaji (upstream regulator) (Tanzania Petroleum Authority or National Hydrocarbons Authority) na lingine kuwa Kampuni ya kibiashara ya Mafuta na Gesi (National Oil and Gas Company) ambapo kila sehemu ya

Muungano itakuwa na Kampuni yake na kuondoa malalamiko ya sasa juu ya Mafuta na Gesi. Pendekezo hili Serikali haijalitolea majibu wala utaratibu wa kulitekeleza ili kuboresha usimamizi wa sekta ya Gesi na Mafuta. Vile vile Pendekezo hili litaweka msingi wa Sekta ya Mafuta na Gesi kusimamiwa na chombo cha muungano badala ya sasa ambapo kinasimamiwa na TPDC ambayo sio Shirika la Muungano. Pendekezo hili litekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni jambo la umuhimu mkubwa kwa Serikali kuzingatia maelekezo ya Kamati kama yalivyokuwa yametolewa hapo awali na kuazimiwa kwa azimio la bunge lako tukufu tarehe 21 Aprili, 2010, kwa kuyafanyia kazi kwa haraka ili kukamilisha maudhui ya Kamati katika kufanikisha mchango wa Mashirika ya umma kwa maendeleo ya Taifa letu.

d) kufanya Tathimini ya Ufanisi wa Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma katika kutekeleza jukumu lake lililopo katika fasili ya 13(d) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2007, iliendelea kufanya Tathimini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma kuangalia iwapo Mashirika hayo yanatimiza malengo ya uanzishwaji wake. Kwa muhtasari Tathimini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma imebainisha

mambo kadhaa katika mashirika yafuatayo,

1. Mamlaka ya Usambazaji maji Dar es salaam (DAWASA)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usambazaji maji Dar es salaam (DAWASA) imeendelea kuwa na matatizo makubwa ya kiutendaji hali inayozorotesha ufanisi wa Shirika hilo muhimu kwa Wananchi.

DAWASA imepata hasara ya jumla ya Shilingi bilioni 26.6 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2008 ukilinganisha na hasara ya shilingi Bilioni 10.4 kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2007, hali hii ni hatari kwa uwepo wa Shirika kwa siku zijazo kama hatua ya kudhibiti upoteaji wa maji. Kamati imejulishwa kwamba 57% ya maji yanayozalishwa Dar es Salaam hupotea ilhali wananchi wanapata kero kubwa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Kwa wakazi wa Dar es Salaam wanaotumia maji ya kununua kwenye madumu, gharama za maji ni kubwa kuliko wananchi wanaotumia maji ya DAWASCO. Utafiti wa Shirika la Water Aid unaonyesha kuwa mwananchi wa kawaida masikini wa Manzese analipia gharama za maji mara kumi na tano zaidi kuliko mwananchi mwenye uwezo wa Masaki! Kamati imelitaka Shirika la DAWASA kurekebisha mara moja hali hii na hasa eneo la upoteaji wa maji kama ilivyoainishwa hapo juu.

2. Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN) kwa mwaka wa fedha 2008/2009 limelimbikiza madeni yanayofikia shilingi bilioni 2.6 na ufanisi kimapato ulishuka kwa kukusanya shilingi bilioni

8.0 ukilinganisha na shilingi 11.5 bilioni zilizokusudiwa kukusanywa hii ikiwa ni tofauti ya asilimia 31% ya lengo kusudiwa. Kamati imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua upya hesabu za TSN kufuatia kutoridhishwa na mahesabu na hata utendaji wa Shirika.

Ni maoni ya Kamati kuwa Shirika hili liongeze juhudi katika ukusanyaji madeni na pia kuzingatia Sheria ya manunuzi na kuepukana na ukiukaji wa Sheria katika manunuzi ya magari chakavu kwa gharama kubwa. Kwa kuwa Serikali inamiliki asilimia 100 katika Shirika hili na ili kuhakikisha TSN inakuwa ni mali ya Umma badala ya Mali ya Serikali (public newspapers badala ya government newspapers) na kwamba Shirika linaweza kujiendesha kwa Faida, basi asilimia 50 ya Hisa za TSN ziuzwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaa haraka iwezekanavyo. Hii itaongeza ufanisi wa Shirika na kuwa kisemeo cha wananchi badala ya sasa ambapo Taifa linapata habari za Magazeti binafsi na ya Serikali pekee. Tunashauri TSN ichapishe magazeti ya Umma kwa kuruhusu umma kumiliki sehemu ya Shirika hili.

3. Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Huduma za Meli imeendelea kutoa huduma katika maeneo ya Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Kamati inaipongeza kwa dhati Kampuni ya Huduma za Meli ambayo imejiendesha kwa muda mrefu bila kupata ruzuku ya serikali licha ya kwamba ipo kwenye orodha ya Mashirika ya kuuzwa (specified). Hata hivyo Kampuni hii ina changamoto nyingi sana ikiwemo ya uchakavu wa Meli, kunyang’anywa mali zake na kupewa

Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kutofanywa maamuzi kuhusu hatma ya Shirika.

Mheshimiwa Spika,Kampuni hii iliwekwa chini ya usimamizi wa CHC ili ibinafsishwe mwaka 1998, lakini hadi leo Serikali haijachukua maamuzi juu ya hatma ya Kampuni hii ili kuipa ufanisi. Kamati inaitaka Serikali kufanya maamuzi juu ya Kampuni hii ili wananchi wanaotumia usafiri wa Maji wapate huduma stahili na bora.

e) Kufuatalia sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ilianza kutekelezwa Nchini ikiwa ni malengo ya kutekeleza mipango ya kiuchumi katika kuongeza uwekezaji na kukuza uchumi chini ya mpango ujulikanao kama ***(Structural adjastument Programme SAP)*** ili kuinua sekta binafsi na kuipa serikali nafasi ya kutekeleza mipango muhimu ya kisera.

Katika utekelezaji wa sera ya Ubinfsishaji na kwa kuzingatia Tathmini iliyofanywa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/ 2009 , Kamati ilibaini kuwa kuna mambo yanatakiwa kufanyiwa kazi na serikali kama ifuatavyo;

- Urejeshaji wa umiliki wa mgodi wa Kiwira uliokuwa umebinafsishwa hapo awali kwa Serikali kuingia ubia na Kampuni ya Tancoal Power (serikali ikimiliki hisa 30%) bado haujakamilika. Kamati ilitembelea mgodi huu mnamo mwezi Machi 2011 na kujiridhisha kuwa Serikali inatakiwa kukamilisha mchakato wa kurudisha Mgodi huu ili apatikane mwekezaji

mwingine aanze kuzalisha makaa ya mawe na umeme mapema iwezekanavyo.

- Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma (CHC) litamaliza muda wake kisheria tarehe 30 Juni , 2011, ni vema Serikali ikafanya uamuzi wa haraka na wa makusudi kuliongezea muda Shirika hili ili kulipa nafasi ya kukamilisha utelezaji wa majukumu yaliosalia ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa madeni ambayo Serikali inayadai kwa baadhi ya Mashirika yaliyobinafsishwa yanayofikia shilingi bilioni 23,610,024,841 hadi tarehe 28/02/2011. Ni vema Serikali izingatie kwamba bado kuna Mali ambazo CHC inazisimamia na kuna watu wengi wanadaiwa kutokana na kununua Mashirika ya Umma na Mali zake bila kulipia kikamilifu. Mabadiliko ya Sheria ya CHC yasiweke kikomo cha muda wa Shirika bali kikomo kiwe ni kazi kukamilika. Kamati inatahadharisha kwamba kuiacha CHC kumaliza muda bila kukamilisha majukumu yake kunaweza kupelekea upoteaji mkubwa sana wa mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma imetumia nyenzo na mbinu zifuatazo kama msingi na muongozo wa utekelezaji wa majukumu yake:

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho) mara kwa mara na hasa kuhusu mamlaka ya Bunge na Kamati zake (Ibara ya 63 ya Katiba na ibara nyingine husika).

b) Kanuni za Bunge (Toleo la Mwaka 2007)

c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (kwa Mwaka ulioishia 30 Juni, 2009)

d) Sheria ya Manunuzi ya umma ya Mwaka 2004, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001, na Sheria iliyoanzisha kila Shirika husika.

e) Taarifa za Msajili wa Hazina

f) Taarifa za mahesabu za kila Shirika kwa Mwaka wa Fedha unaojadiliwa ikiambatanishwa na majibu ya hoja za Ukaguzi kutoka katika Manejimenti ya kila Shirika lililojadiliwa na ,

g) Taarifa za kitafiti kutoka maeneo mbalimbali juu ya mambo yanayogusa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali ili kutekeleza wajibu wake, zikiwemo:

i) Semina za mafunzo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Msajili wa Hazina. Lengo la semina hizi za mafunzo lilikuwa ni kupata taaluma ya jinsi ya kusoma na kutafsiri mahesabu.

ii) Kujadili na kuchambua taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika mbalimbali kwa kuwaita Maafisa Masuhuli (Accounting Officers na Wenyeviti wa Bodi mbele ya Kamati)

iii) Kufanya ziara za kujiridhisha na thamani na uhakika wa kuwepo kwa miradi /mashirika husika (value for money audit and expenditure katika miradi iliyo chini ya Shirika la

Maendeleo la Taifa (NDC) ya Mchuchuma, Liganga na South Ngaka na pia mradi wa Kiwira ambayo inategemewa kuwa ukombozi wa sekta ya umeme na viwanda kwa Taifa letu kwa siku za hivi karibuni.

iv) Kuunda kamati ndogo ili kufuatilia masuala ambayo Kamati ilihitaji maelezo ya kina kuhusiana na Hesabu za Shirika husika. Kwa Mfano: Kamati Ndogo imeundwa kufuatilia ubinafsishwaji na hatma ya kampuni ya General Tyre East Africa Limited ambayo imeshindwa kufanya kazi na kwa kuzingatia ukweli kuwa Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 74 katika Kampuni hiyo.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI NA MAELEZO YA KAMATI KUHUSU MASHIRIKA

2.1. Taarifa ya Uwekezaji na hali halisi ya Mitaji ya Umma katika Mashirika

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kwa Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2009 ulibaini kuwa kwa kipindi hicho kulikuwapo na jumla ya Mashirika ya umma 196 yaliyo hai na Mashirika 18 ambayo yalikuwa kwenye hatua mbalimbali aidha kufunga shughuli zake, kubinafsishwa,kuundwa upya au kufilisiwa. umiliki wa hisa za Serikali ulikuwa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Serikali iliwekeza kiasi cha Shilingi 6,143,567,862,966.68 katika mashirika ya Umma. Mtiririko wa gawio kwa muda wa miaka miwili ulikuwa kama ifuatavyo:

Mwaka	**Mtaji uliowekezwa**	**Gawio lililopatikana**
2007/2008	5,140,499,602,257.00	76,951,126,934.16
2008/2009	6,143,567,862,966.68	31,223,253,590.26

Chanzo cha Taarifa: Maelezo ya Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya umma yaliweza kuchangia mapato serikalini kutokana na gawio, mikopo na riba na michango mingine. Gawio kutoka Mashirika ya Umma limepungua kutoka Shilingi 76,951,126,934.16 Bilioni mwaka 2007/2008 mpaka shilingi bilioni

31,223,253,590.26 Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, gawio na michango mingine (remittances) inategemea sana utendaji wa Mashirika ya Umma kwa mwaka husika. Kupungua kwa gawio na michango mingine kutoka mashirika ya Umma kwenda serikalini ni ishara kuwa Mashirika ya umma yamepungua ufanisi na hivyo kupata hasara. Kamati inaendelea kumtaka Msajili wa Hazina aimarishe usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yafanye kazi kwa ufanisi na kutoa faida kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, yapo Mashirika ambayo serikali inashikilia hisa za asilimia 50 na chini ya hapo hayana usimamizi *(oversight*) wa kibunge.Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hwana Mamlaka ya kukagua hesabu hizo na hivyo Kamati hii haikupata fursa ya kujadili taarifa za hesabu zao na hatimae kutokujua mtaji wa umma unaendeshwa namna gani. Mashirika hayo na hisa zilizopo ni kama ifutavyo;

- BP (hisa 50%)
- Zain Tanzania (hisa 40%)
- Abood soap industries (hisa 23%)
- NBC (hisa 30%)
- Kilombero Sugar (hisa 25%)

2.2 MATATIZO SUGU YALIYOIBULIWA KWENYE MASHIRIKA YA UMMA KWA MUJIBU WA TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA JUNI 30, 2009.

Mheshimiwa Spika, Ukurasa wa 111 wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha ulioishia juni 30, 2009 yameainishwa mambo yanayo changia kurudisha nyuma utendaji wa Mashirika ya umma na taasisi umma Nchini kuwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji ya kutosha kwa shughuli za Mashirika husika, uongozi usio imara katika mashirika hayo, kutowajibika ipasavyo kwa bodi za wakurugenzi, mapungufu katika mipango kazi ya mashirika, mapungufu katika kuzingatia taratibu za manunuzi na utunzaji wa mali za Mashirika hayo. Kamati ilifanya juhudi sana katika kufuatilia na kutoa maagizo kwa mashirika mbalimbali yaliobainika kuwa na aina hiyo ya udhaifu.

Kamati pia imefanya tathmini na kubaini Matatizo sugu katika Mashirika yetu ya Umma kama ifuatavyo:

1) **Uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma**

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa mambo yanayotatiza ufanisi katika Mashirika ya umma ni kutowajibika ipasavyo kwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika ambazo kimsingi ndio zimekabidhiwa jukumu la kuhakikisha utendaji wa Mashirika

unakuwa na ufanisi.

Kamati ilibaini kuwa katika baadhi ya Mashirika wajumbe wa Bodi wamekuwa hawazisimamii Menejimenti za Mashirika yao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuziacha Menejimenti zikitekeleza majukumu ya Bodi za Wakurugenzi hali inayoondoa dhana nzima ya uwajibikaji katika Mashirika ya umma.

Ni ushauri wa Kamati kuwa imefika wakati muafaka sasa kwa serikali kuingia mikataba ya utendaji (performance contracts) na Wajumbe wa Bodi za Mashirika ili kupima utendaji wao kwenye bodi husika na pale pasipokuwa na ufanisi Wajumbe hao wa Bodi waondolewe.

2) **Mashirika ya Umma kutokuwa na Mipango ya Manunuzi kwa mwaka *(Annual Procurement Plans)* na Vitengo vya Manunuzi *(Procurement Management Units)***

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sehemu ambazo kiasi kikubwa cha fedha za umma zinapotea ni katika suala zima la manunuzi. Hivyo kusipokuwa na udhibiti wa kutosha eneo hili litaendelea kupoteza fedha nyingi za umma na kwa muda mrefu kubainishwa kama chanzo kikubwa cha sifa mbaya ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika mashirika na serikali kwa ujumla. Ni ushauri wa Kamati kwamba Sheria na taratibu zote za manunuzi zinapaswa kuzingatiwa. Mifano michache ya manunuzi yasiyozingatia Sheria katika manunuzi ya Umma ni pamoja na :

- Ununuzi wa magari yaliyokwisha tumika uliofanywa na Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN) kinyume na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 ikiwamo ununuzi wa gari

aina ya NOAH kwa gharama ya shilingi milioni 30 bei isiyokuwa halisi kwa soko hivyo kulinyima shirika thamani ya fedha inayolipwa.

- Manunuzi ya magari yalifanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa jumla ya shilingi 102,285,441 bila kufuata sheria ya manunuzi
- Mamlaka ya kudhibiti Mawasiliano (TCRA) iliingia zabuni ya kupitia muundo wa ofisi, tathmini ya utendaji kazi na kupitia ngazi za mishahara“organisation review, job evaluation, na job grading” ambayo awali ilitangazwa tarehe 16, 17 na 20 Agusti 2007 na kuingia mkataba tarehe 28 Januari 2008 kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Tathmini (Evaluation Committee).

3) Mashirika kutokutunza taarifa ya mali zao ipasavyo

Mheshimiwa Spika,utunzaji wa mali za kudumu za Mashirika (fixed register) na kuziweka katika kumbukumbu ili zitumike pale zinapohitajika imekuwa ni zoezi gumu kwa mashirika mengi ya Umma. Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa matokeo ya kutokuwa na rejesta za mali za kudumu unaweza kusananisha upotevu au wizi wa mali ya umma kama hatua za haraka hazitachukuliwa kwa kuboresha mifumo ya utunzaji kumbukumbu ya mali kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Miongoni mwa Mashirika yaliyobainika kuwa na tatizo hilo ni pamoja na Kampuni ya simu Tanzania (TTCL) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

4) Mashirika na Taasisi kukosa mitaji ya kujiendesha

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Umma yana matatizo makubwa sana ya mitaji ya kuwekeza (recapitalization). Kukosekana kwa mtaji kunaathiri Mashirika ya Umma kuendeshwa kwa ufanisi. Mashirika yaliyoathiriwa zaidi na tatizo hili na kiasi cha mtaji wanachohitaji kwa sasa ili kujiendesha ni kama ifuatavyo,

S/N	SHIRIKA	KIASI CHA MTAJI KINACHOHITAJIKA
1.	Shrika la Umeme Tanzania (TANESCO)	Milioni 2,877,586.82
2.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Bilioni 1.5
3.	Shirika la maendeleo la Taifa (NDC)	Bilioni 4.8
4.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Bilioni 169
5.	Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)	Bilioni 2.4
6.	Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)	Bilioni 18.2

Mheshimiwa Spika, Tatizo hili bado linaendelea. Hivyo, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuyaongezea mashirika hayo mitaji ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hata hivyo ipo haja ya Bunge kujiridhisha na sababu za kupungua kwa mitaji ya Mashirika hayo. Hoja ya Kuanzishwa kwa Tanzania Public Investments Fund kutasaidia sana kumaliza tatizo hili la mitaji kwa Mashirika ya Umma.

5) Tatizo la ucheleweshaji wa michango toka kwa wanachama unaofanywa na waajiri kwenda kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kuna taasisi za serikali na hasa wizara ambazo zimekuwa mara kwa mara zikichelewesha kuwasilisha michango ya kisheria kama waajiri kwa Mifuko ya Pensheni.

Ucheleweshaji huu wa kuwasilisha malipo ya kisheria kwenye mifuko ya Pensheni sio tu unatatiza utendaji wa mifuko ya pensheni lakini pia unawanyima watumishi husika haki zao za kisheria za kupata malipo pindi watakapostaafu tatizo ambalo limewakumba wastaafu wetu wengi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kwa mfano Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2008 ulikuwa unazidai Wizara zifuatazo kiasi kikubwa cha fedha ambazo hazikuwasilishwa kwa muda mwafaka;

Na.	WIZARA/ IDARA	KIASI INACHODAIWA (Tshs)
1.	Afya na Ustawi wa Jamii	413,560,330
2.	Elimu na Mafunzo ya Ufundi	386,841,586
3.	Mifugo	113,050,717
4.	Kilimo na Chakula	69,361,728

5.	Mahakama	53,230,902
6.	Mali asili na utalii	46,122,503

6) Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kuhusu Mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2009 katika sehemu ya utangulizi wa taarifa yake, alibainisha jambo hili kama kikwazo cha uwajibikaji katika Mashirika ya Umma.

Kwa kuzingatia dhana ya Utawala Bora na Misingi ya uhuru wa Bunge kama muhimili wa kuisimamia Serikali ni vema kabisa waheshimiwa wabunge wakawa huru nje ya Bodi za Mashirika ya umma ili watekeleze wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kwa ukamilifu. Kamati inampongeza kwa dhati Gavana wa Benki kuu wa kutoa muongozo wa kuwaondoa Waheshimiwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Taasisi za fedha hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa Mamlaka mbali mbali za uteuzi zimeendelea kuteua waheshimiwa wabunge kuwepo kwenye bodi za Mashirika ya umma, baadhi ya mashirika ambayo waheshimiwa wabunge ni wajumbe wa bodi ni kama ifuatavyo, TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mfuko wa Pensheni ya watumishi wa umma.

7) Mashirika ya Umma kutoweka kumbu kumbu za Mali zao ipasavyo

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kubaini kuwa kuna baadhi ya Mashirika ya umma yameshindwa kuweka kumbu kumbu sahihi za mali zao hali inayochangia upotevu wa mapato. Kwa mfano katika chuo cha usimamizi wa fedha (IFM) idadi ya wanafunzi waliopo kwenye ledgers na idara ya uhasibu zinatofautiana.

Tatizo hili kwa chuo cha usimamizi wa fedha limesababisha kutokusanya ada za wanafuznzi kwa ukamilifu ikiwa ni pamoja na madeni ya malipo mbali mbali yaliyotakiwa kufanywa kwa mujibu wa sheria.

8) Michango ya Wanachama kutowekewa takwimu sahihi na Mifuko ya Pensheni (Unallocated contributions)

Mheshimiwa Spika,tatizo la Michango inayopokelewa kutoka kwa Waajiri kwenda kwenye Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii kutowekwa Takwimu Sahihi kwa wakati Muafaka limeendelea kujitokeza kwenye mifuko ya pensheni ya PPF, NSSF na PSPF kwa muda mrefu sasa.

Uchunguzi wa kamati umebaini kuwa fedha hizi zinapopokelewa na kutowekwa takwimu Sahihi za mahali zinapotoka zimekuwa zikiandikwa kama ***unallocated funds*** hali inayoweza kusababisha upotevu wa Fedha za wanachama wa mifuko husika hasa watakapokuwa wanastaafu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kwa mfano katika Mfuko wa PSPF suala la Fedha kutokufika kwa takwimu sahihi limekuwa likibebeshwa kama mzigo wa mwanachama na sio mwajiri, Kamati

ilichukua hatua mara moja ya kuzuia vitendo vyovyote vitakavyofanyika kuwanyanyasa wanachama wa mifuko kwa makosa yanayofanywa na Waajiri na badala yake Mifuko ya Hifadhi za Jamii imeagizwa kufanya jitihada za kutunza kumbu kumbu za wanachama wao kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, jedwali lifuatalo linaainisha Fedha zilizoshindwa kuwekewa takwimu sahihi na Mifuko ya Pensheni;

S/N	MFUKO	UNALLOCATED CLAIMS/RECIAVABLES
1.	PPF	1,673,514,000 (Tarehe 07.10.2008)
2.	PSPF	148,993,261 (Tarehe 30.06.2009)

9) Malipo kwa Watumishi wa Mkataba kinyume na Taratibu za Utumishi wa umma kwa wafanyakazi wa mfuko wa PPF

Mheshimiwa Spika, Mashirika mbali mbali ya Umma yamekuwa yakilipa mafao tofauti tofauti kwa Watumishi wao kutokana na mikataba ya ajira inavyoainisha, aidha kumekuwapo na mifumo kadhaa ya kutoa motisha kwa watumishi ili kuwapa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya Mashirika yanalipa mafao hayo kinyume na Sheria za Utumishi wa Umma na pia sheria za Kodi ya Mapato hali inayosababisha baadhi ya watumishi kupata mafao mara mbili (double benefits) kinyume na sheria ya mafao kwa watumishi wa umma. Mfumo wa Kiinua mgongo **(gratuity)** na endowment scheme ni mifumo ambayo inatumika sana hivi kwenye

Mashirika ya Umma. **Gratuity na Endowment** kwa pamoja ni makosa kimaadili, kwa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini katika mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) kuwa kuna Watumishi wa Mkataba wanaopata malipo ya gratuity pindi wamalizapo mikataba yao ya kazi na pia hulipwa Pensheni wanayochangiwa na kuchangia kila mwezi na zaidi hulipwa pia Mafao ya endowment scheme. Mapungufu makubwa yaliyogunduliwa na Kamati katika jambo hili ni kuwa kumekuwa na Utekelezwaji wa sheria za mafao ya aina mbili kwa wakati mmoja kinyume cha sheria na pia ilibainika kuwa ni kada ya watumishi wa ngazi ya menejimenti tu ndio wanaofaidika na mfumo huu na sio watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na tatizo hilo Kamati ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kwa kushirikaiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya uchunguzi wa malipo ya fedha hizo kwa kuanzia na PPF na Mifuko mingine yote ya Pensheni na katika Mashirika mengine ya Umma ili kuhakisha uhalali wa kisheria wa malipo hayo na kisha kutoa muongozo kwa Mashirika yote ya jinsi ya kulipa mafao kwa watumishi wao kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma na Kodi ya Mapato. Uchunguzi huu maalumu utakaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara utakapokamilika na kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati itatoa taarifa rasmi hapa Bungeni na kupendekeza hatua za kuchukua ili kudhibiti hali hii ambayo imeanza kushika kasi miongoni mwa Mashirika ya Umma.

10) Udhamini wa Serikali kwa Mashirika na Makampuni binafsi kukopa kwenye Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya pili mfululizo Kamati ya POAC inawasilisha Bungeni ushauri wa kuitaka Serikali kuacha kutoa udhamini kwa taasisi zake na mara nyingine kwa Kampuni binafsi ili zipate mikopo toka kwenye Mashirika ya Umma, uzoefu wa Kamati umeonyesha kuwa baadhi ya mikopo yenye udhamini wa serikali hailipwi kwa wakati na muda mwingine hailipwi kabisa hali inayoweza kusababisha Mashirika ya Umma kufa, Baadhi ya mikopo ya namna hiyo ni kama ifuatavyo,

- Mkopo wa shilingi bilioni 53 toka PSPF kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu
- Mkopo wa bilioni 14.1 pamoja na riba toka NSSF kwenda General Tyre
- Mkopo wa shilingi 12 bilioni toka NSSF kwenda TanPower Resources (Kiwira)

Mheshimiwa Spika, urejeshaji wa mikopo hiyo umekuwa mgumu na wa kusua sua sana hali inayohatarisha usalama wa fedha za umma kwa siku zijazo.

2.3 KUFUATILIA SERA YA UBINAFSISHAJI

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati ya Bunge ya Hesabu za mashirika ya Umma imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kwa mujibu wa kanuni za Bunge, fasili ya 13(e) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni Toleo la mwaka 2007. Katika eneo hili Kamati inatoa taarifa kuhusu jinsi ilivyotekeleza wajibu huu kwa kuzingatia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ripoti ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kwamba mpaka mwezi Juni 30, 2009 mashirika 277 na vitengo 366 vilikuwa vimebinafsishwa na mikataba ya mauzo kusainiwa au makampuni hayo kupelekwa kwa mfilisi. Katika kipindi hicho serikali ilipata mapato ya jumla ya shilingi 6.7 bilioni kutokana na ubinafsishaji huo. Vilevile serikali bado inadai baadhi ya wawekezaji jumla ya shilingi 110.1 bilioni ikiwa ni pamoja na mikopo iliyotolewa wakati wa ubinafsishaji ambayo ni shilingi bilioni 93.4.

Mheshimiwa Spika,kwa mujibu wa tathimini iliyofanywa na shirika hodhi la yaliyokuwa mashirika ya umma (CHC) hadi kufikia 30 juni,2009 kwa mashirika 62 yaliyobinafsishwa ni mashirika 12 tu ndiyo yalikuwa yanaendelea vizuri na uzalishaji, mashirika 27 yalikuwa katika hali ya wastani kiutendaji na mashirika 23 yalikuwa yamefunga shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikamilishe Tathimini ya Mashirika yaliyobinafsishwa ili taarifa kamili iwasilishwe mbele ya Bunge.

2.4 TATHMINI YA UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa na utaratibu wa kupima ufanisi wa Mashirika ya Umma kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- Utendaji halisi wa Shirika katika kufikia malengo ya kimsingi yanayowekwa na shirika lenyewe kwa mujibu wa sheria ama taratibu zinazotawala kuanzishwa kwa shirika hilo.
- Uwezo wa kifedha wa Shirika. Uwezo wa kifedha wa Shirika hupimwa kwa kuangalia faida au hasara inayopatikana katika mwaka husika wa utendaji wa shirika.
- Uwezo wa shirika katika kurekebisha hasara zinazojitokeza
- Uzingatiaji wa mtizamo wa C Tano ***(Corporate good governance, Capitalization, Compliance with laws, Competency of Managers, Corruption free and collussion)***

Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba ufanisi wa mashirika huathiriwa na Mambo makubwa matatu.

Moja ni Mikakati hafifu ya Mashirika yenyewe katika kutekeleza majukumu yake, mbili ni mwenendo ama maamuzi ya Serikali Kuu juu ya Mashirika hayo (kwa Mfano Serikali kuendelea kukopa kiasi kikubwa cha fedha kutoka katika mashirika ya hifadhi, mashirika kukaa kwa muda mrefu bila Bodi za Wadhamini kwa mfano hadi tarehe 30 machi 2010 Mashirika yafuatayo yalikuwa hayana Bodi za Wadhamini hivyo kuyapunguzia uwezo wa kufanya kazi ipasavyo; Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Bodi ya Tumbaku Tanzania,Bodi ya Utalii Tanzania nk, Mashirika kuwa chini ya watu wanaokaimu madaraka

kwa muda mrefu, nk). Tatu ni athari zinazotokana na mabadiliko mbalmbali katika mazingira ya dunia kwa ujumla (Mfano Mdororo wa Uchumi Duniani) ambao umeathiri sana Mashirika ya TANAPA na Ngorongoro.

Tathmini ifuatayo ilifanyika katika mashirika mahususi kama inavyojieleza,

2.4.1 Kampuni ya ndege ya Tanzania (ATCL)

Mheshimiwa Spika,Tathmini ya ufanisi katika kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ilibaini mambo yafuatayo ambayo yamesababisha Kampuni hii kushindwa kabisa kujiendesha,

- Kampuni inakabiliwa na madeni yanayofikia shilingi 23.3 bilioni
- Kampuni ina mtaji hasi wa shilingi 14 bilioni
- Kuanzia mwaka 2007/2008 serikali ilisitisha rasmi utoaji wa ruzuku ya shilingi milioni 500 kwa mwezi kwa ATCL hivyo kuiacha Kampuni bila msaada au ruzuku yoyote.
- Kwa zaidi ya miaka mitano sasa Serikali imetafuta mwekezaji wa kuwekeza kwenye ATCL bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, jitihada za makusudi zinatakiwa kufanywa ili kuiokoa ATCL ili hata kama mwekezaji atapatikana aikute Kampuni ikiwa inajiendesha, Kamati imetoa mapendekezo yake kuhusu ufufuaji wa ATCL kwenye sehemu ya maoni katika taarifa hii.

2.4.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, tarehe 28/03/2011 Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ili kujadili Taarifa ya Hesabu za Shirika kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Kamati ilibaini kuwa Taarifa ya Hesabu za TANESCO hazijasainiwa na Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za serikali (CAG) sababu ikiwa ni deni la shilingi bilioni 94.0 zinazodaiwa na Dowans (contigent liability) hivyo CAG alihitaji kujiridhisha na vitabu ambavyo deni hilo lingepaswa kuonekana.

Baada ya kikao hicho Kamati iliazimia kufanya kikao cha pamoja na Makatibu wakuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na ile ya Nishati na madini pamoja na Bodi ya TANESCO ili kufikia mwafaka kuhusu Contigenty liability hiyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Machi, 2011 Kamati ilikutana Makatibu wakuu wa Wizara ya Fedha na Nishati na Madini pia na Bodi ya TANESCO na Mwakilishi wa CAG kwa majadiliano ya kina ikiwa ni pamoja na kupokea taarifa muhimu kuhusiana na contigent liability ya shilingi 94.0 bilioni. Baada ya majadiliano ya kina Kamati iliazimia kuwa ni vema deni hilo lisitokee katika vitabu vya Hesabu za TANESCO kama Mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyokuwa amependekeza hapo awali kutokana mazingira ya uingiaji mkataba husika.

2.4.3 Kampuni ya General tyre East Africa Limited (GTEAL)

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ilianzishwa mwaka 1969 ikiwa ni ubia wa Serikali ya Tanzania na General Tyre USA baadaye Kampuni ya General Tyre USA iliuza hisa zake kwa Kampuni ya kijerumani ya Continental AG serikali ikiwa inamiliki Hisa 74% na Continental AG asilimia 26%.

Kiwanda kilijiendesha kwa faida hadi mwaka 1997 kilipoanza kupata hasara na kuwa na madeni makubwa na kiasi cha kufikia hatua ya

kufungwa kutokana na ushindani wa kibiashara, tokea mwaka 2008 Serikali iliendelea kufanya jitihada kufufua kiwanda hiki wa kushirikiana na mwanahisa mwenza bila mafanikio yoyote hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa jitihada hizo zimeonekana kugonga mwamba na kwa kuzingatia uwekezaji wa Umma uliofanyika katika kiwanda hicho na Taarifa zilizopo kwenye Kamati, kamati imeamua kuunda Kamati ndogo yenye wajumbe wafutao ili kwa kushirikiana na Wataalamu wa ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya CHC kuchunguza mambo kadhaa ndani ya GTEAL, wajumbe wa Kamati hiyo ni;

1. Mhe. Muhamad Chomboh, Mb
2. Mhe. Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mb
3. Mhe. Esther Matiko, Mb.
4. Wajumbe wawili kutoka Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara
5. Katibu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ndogo ya Bunge imeazimia na kukubaliana kutekeleza Hadidu zifuatazo za Rejea katika uchunguzi wao kuhusu GTEAL;

1. Kufuatilia Mkopo kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wenye jumla ya dola za kimarekani milioni kumi (10 million USD) uliotolewa kwa GTEAL na kuona kama taratibu zilifutwa kutoa wakati wa kutoa mkopo huu.
2. Kufuatilia matumizi ya mkopo kama yalitumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kama yalitumika ilikuwaje kiwanda

kisimame kufanya kazi muda mfupi tu baada ya kupokea fedha za mkopo.

3. Kufuatilia sababu zilizoifanya GTEAL kujiendesha kwa hasara na sababu za mwekezaji kushindwa kukataa kutoa mkopo.
4. Kufuatilia mali za Kampuni na hali ya mali hizo kwa sasa.
5. Kufuatilia msimamo wa Serikali kuhusu kufilisi Kampuni na sababu za kufikia msimamo huo na kama kuna maslahi kwa umma.
6. Kutoa mapendekezo ya namna ya kufufua kampuni.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati hii ndogo , uchambuzi na maoni yake kwa ufasaha yatawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu mapema kwa kadiri itakavyowezekana ili kutatua tatizo hilo.

2.4.5 Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa umma(PSPF)

Mheshimiwa Spika,Tathimini iliyofanyika katika mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya umma (PSPF) ulibaini tatizo kubwa la madeni ambayo Mfuko unaidai , Serikali mengi yakiwa ni ya siku za nyuma kabla ya mwaka 1999 ambapo baadhi ya watumishi wa umma walitakiwa kulipwa pensheni lakini hawakuwa wakichangia kwenye mifuko ya Hifadhi za jamii hivyo Serikali ikachukua deni hilo la shilingi trilioni 2.6 na shilingi bilioni 719 ambazo PSPF imekwisha lipa wastaafu baada ya kuanzishwa kwake.

Baada ya kupokea hoja za ukaguzi za taarifa ya hesabu ya PSPF, Kamati ilipata wasi wasi juu ya ukubwa wa deni hilo na hivyo kuamua kukutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na uchumi ili kulijadili deni hilo kwa kina.

Mheshimiwa Spika, Kikao hicho muhimu kilifanyika tarehe 25/03/2011 ambapo majadiliano hayo yalizaa matunda, Kamati inapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilianza mara moja kulipa deni hilo na kwa mwezi Machi 2011 Serikali imeilipa PSPF shilingi bilioni 30 kwa bajeti ya mwaka 2009/2010 na imetoa uthibitisho wa kuendelea kulipa deni hilo kwa kutenga kipaumbele katika bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya ufanisi wa Mashirika ya umma imebaini tatizo la nafasi za juu katika Mashirika kama CHC, PSPF na TANESCO kuwa zinakaimiwa na maafisa wengine kwa muda mrefu hali inayoweza kuzorotesha ufanisi katika mashirika hayo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAFANIKIO YALIOKWISHAPATIKANA KUTOKANA NA KAZI ZA KAMATI

Mheshimiwa Spika, katika kujadili taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma, Kamati imebaini kuwa yapo Mafanikio na Changamoto mbalimbali ambazo Mashirika hayo yanakabiliana nazo. Kwa mfano: Suala la upungufu wa Mitaji ya kutosha kutekeleza mipango ya kila Mwaka ya Mashirika, baadhi ya mashirika kukosekana kwenye Orodha ya Msajili wa Hazina hivyo kumnyima fursa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulikagua Shirika, kuwepo maelekezo ya Serikali yanayo athiri utekelezaji wa mipango mkakati ya Mashirika, kutofautiana kwa kiasi kikubwa kwa viwango vya posho zinazolipwa na mashirika, kuchelewa kuundwa kwa Bodi za Wadhamini/ Wakurugenzi wa baadhi ya Mashirika na baadhi ya Watendaji katika nafasi muhimu za Mashirika kukaimu kwa muda mrefu (mfano CHC, PSPF), Ni katika mazingira ya changamoto hizi ambapo Kamati inapenda kutoa ushauri wake kwa ajili ya maboresho katika ufanisi wa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni yetu juu ya mambo yaliyotajwa hapo juu, ni vema nikatoa maelezo machache juu ya mafanikio ambayo Kamati imeyapata tokea kuanzishwa kwake kwa yana:

i. Utendaji kazi wa Kamati umeweza kuyakumbusha Mashirika kuhusu uwepo wa uangalizi (oversight) wa Bunge katika nidhamu ya matumizi ya fedha na raslimali za

umma. Hali hii ni tofauti na nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma iliyokuwepo katika mashirika kabla ya Kamati hii kuundwa.

ii. Kamati imehakikisha kuwa Serikali inaanza kulipa deni inalodaiwa na na mfuko wa pensheni ya watumishi wa serikali PSPF, kwa mwaka huu wa fedha bilioni 30 zimelipwa mwezi machi 2011 baada ya Kamati kuagiza hivyo.

iii. Kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali, Msajili wa Hazina na wadau mbalimbali wa Maendeleo, Kamati imeweza kuandaa Makongamano kadhaa ya kujadili mwenendo wa mashirika kiutendaji kwa lengo la kutambua matatizo yanayoyakabili na kupendekeza kwa Serikali namna bora ya kutatua matatizo hayo.

iv. Kamati imesaidia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kufutiwa Malimbikizo na riba waliyokuwa wanadaiwa na Mfuko wa PPF zaidi ya Shilingi Milioni 600 na sasa wanalipa makato ya kisheria kwa muda Mwafaka.

v. Kamati imelisaidia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kuharakisha mchakato wa Utekelezaji wa Miradi ya Mchuchuma, liganga na South Ngaka ambayo italisaidia Taifa kuondokana na tatizo la umeme na kuharakisha maendeleo ya Viwanda.

vi. Maagizo ya Kamati yamechangia kwa kiasi kikubwa kuitoa TANESCO kutoka katika mazingira ya kujiendesha kwa

hasara (Mwaka wa 2006/2007 Shirika hilo lilikuwa likiendeshwa kwa nakisi ya Shilingi bilioni 67 mpaka kufikia nakisi ya Shilingi bilioni 5 Mwaka 2008/2009 na kuna uwezakano mkubwa kwa Shirika hili kuanza kupata faida iwapo mgawo wa umeme utamalizika.

vii. Kamati kwa kushirikiana na vyombo vya habari imeongeza uwajibikaji na uwazi katika Mashirika ya Umma kwa kuwahusisha waandishi katika ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Mashirika ya umma ili kujiridhisha na thamani halisi za miradi hiyo.

viii. Maagizo na usimamizi thabiti wa kamati umesaidia kuongezeka kwa hati safi za ukaguzi wa mashirika ya Umma kinyume na miaka iliyopita (Hati Safi 45 kati ya mashirika 51 sawa na asilimia 88 ya Mashirika yaliyokamilisha taarifa za hesabu zao kwa Mwaka 2008/2009)

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

4.1 MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KATIKA MAENEO MBALIMBALI

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo wa kina , Kamati inashauri mambo yafuatayo kutekelezwa na Serikali kwa lengo la kuboresha zaidi hali ya mashirika na taasisi za umma nchini ili zilete tija katika kutoa huduma kwa watanzania na katika kukuuza uchumi wa nchi;

4.1.1 UDHAMINI NA UCHUKUAJI WA MIKOPO KUTOKA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya utaratibu wa kudhamini Makampuni binafsi na Taasisi za Serikali zinazokopa fedha kutoka katika Mashirika mbali mbali ya Umma ili usiwe udhamini wa kufilisi Mashirika. Utekelezwaji wa ushauri huu uende sanjari na Serikali yenyewe kulipa kwa wakati madeni yanayotokana na ukopaji wake wa fedha kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mashirika mengine ya Umma pamoja na kusaini ipasavyo hati zote za makubaliano ya ukopaji wa fedha hizo.

Mifano ya mikopo inayoongelewa hapa ni kama ifuatavyo;

- Mkopo wa shilingi bilioni 53 toka PSPF kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu
- Mkopo wa shilingi bilioni 14.1 pamoja na riba toka NSSF kwenda General tyre
- Mkopo wa shingi 12 bilioni toka NSSF kwenda Tan Power

Resourses (Kiwira)

4.1.2 KUTEKELEZA MAONI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2007/ 2008 aliweza kuainisha maeneo 17 ambayo yana mapungufu mbalimbali na kuwaomba wadau ambao ni Serikali, Bunge na Mashirika husika kuyatekeleza ili kutoa ufanisi kwa mashirika.

Maeneo makubwa yalihusu utawala bora katika Mashirika, Mifumo ya Udhibiti wa ndani, matumizi bora ya rasilimali na uwajibikaji.Kamati imebaini kuwa maeneo mengi bado kushughulikiwa ipasavyo, hivyo Kamati inapendekeaza uwajibikaji wa kutosha katika kutekeleza maoni yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali kwa muda muafaka

4.1.3 UUNDWAJI WA BODI ZA WAKURUGENZI

Bodi za wadhamini ndizo zenye jukumu kubwa katika kusimamia utendaji wa Mashirika ya umma ili kuyapa ufanisi. Kutokuwepo kwa Bodi hizi kwa baadhi ya Mashirika siyo tu kwamba kunaathiri kasi ya maamuzi na utekelezwaji wa mipango mbalimbali ya mashirika hayo bali pia kunaathiri ratiba za utendaji kazi wa Kamati yetu. Kwa mfano kwa mwaka wa taarifa hii, Kamati ilishindwa kujadili taarifa za hesabu za mashirika yafuatayo, Bodi ya Utalii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii nchini kwa sababu hayakuwa na Bodi za wadhamini. Kwa maana nyingine Kamati haina maoni yoyote juu ya hesabu za mashirika

hayo kwa mwaka wa pili mfululizo.

4.1.4 UFANISI WA MAMLAKA ZA MAJI NCHINI

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Mamlaka nyingi za Maji hapa nchini zinafanya kazi kwa kutumia mitandao ya kizamani sana katika kusambaza maji kwa wananchi. Mitandao hiyo imechoka hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha upotevu wa maji yanayosambazwa kwa gharama kubwa (unaccounted water).

Mfano dhahiri ni Kampuni ya Usambazaji Maji Dar es salaam (DAWASA) ambayo kwa mwaka 2008/2009 ilikuwa inapoteza 57% ya maji yote yanayozalishwa.


Kamati imeiomba ofisi ya Taifa ya ukaguzi kufanya ukaguzi maalum kuhusiana na hali hiyo ili kuweza kujenga mkakati utakaozisaidia Mamlaka zote za maji Nchini kuimarisha makusanyo ya mapato yao.

Ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali ijipange kupitia mradi wa maendeleo ya sekta ya maji (WSDP) kuhakikisha mitandao ya maji inakarabatiwa upya ili kutozitia Mamlaka hasara ya kusambaza maji kwa gharama kubwa. Njia mojawapo ya kujipanga ni kwa Serikali kudhamini mikopo kwa Mamlaka za maji ili zifanye uwekezaji mkubwa katika miundo mbinu ya maji ambayo kwa asilimia kubwa ni chakavu.

Ni ushauri wa Kamati pia kwamba ili kuleta ufanisi wa kutosha kwa Mamlaka za maji nchini ni vema Serikali ikaangalia utaratibu wa kulipa ankara za maji kwa taasisi zake kupitia wizara mama za taasisi husika ili kuondoa udhaifu unaoonekana dhahiri kwa Taasisi za Serikali kuzembea kulipa ankara hizo.

4.1.5 SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya mtanzania mmoja mmoja na kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla. Kwa maana hiyo basi ufanisi wa Shirika la Usambazaji na Ugawaji wa Umeme nchini ni muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Shirika hili linayo mipango muhimu sana ambayo ikitekelezwa ipasavyo nchi inaweza kuwa na umeme wa uhakika na wa kutosha. Tatizo lililopo hapa ni ukosefu wa fedha za kutekelezea mipango hiyo.



Mheshimiwa Spika, Ninayo imani kwamba Bunge hili litakubaliana kwa kiasi kikubwa na mtazamo kwamba TANESCO wanafanya kila jitihada kujinasua na hali mbaya ya kifedha kwa kupunguza nakisi

toka bilioni 26 (mwaka 2007) hadi nakisi ya bilioni 5 (mwaka 2008). Kwa msingi huo basi ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali yetu ijipange vya kutosha kuhakikisha kwamba Shirika hili linatafutiwa fedha za kutosha kukamilisha mipango yake. Mojawapo ya vyanzo vya fedha hizi ni kwa serikali kuishawishi Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini kuwekeza katika miradi ya uzalishaji wa umeme nchini kama ilivyo kwa nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ya kuiimarisha TANESCO ni kwa kuhakikisha kuwa Bodi ya Wakurugenzi inatimiza majukumu yake ikiwamo utoaji wa zabuni mbali mbali bila kuingiliwa na mara nyingine kusimamiwa na Wizara mama na Mamlaka nyingine hali inayosababisha utendaji wa TANESCO kuwa duni na hasara kama ilivyojitokeza kwa Kampuni za Richmond na baadae Dowans.

4.1.6 MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII (PENSION SCHEMES)

Mheshimiwa Spika, mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kufanya vizuri kwa muda mrefu na kwa tathimini iliyofanyika hivi karibuni na Wataalamu kutoka benki ya Dunia kwa kushirikiana na Mamlaka ya udhibiti na usimamizi wa sekta ya Hifadhi ya Jamii Nchini (Social Security Reguratory Authority, SSRA) imeeleza wazi kuwa mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendelea vema ila kutoa angalizo sehemu kadhaa za kutiliwa mkazo.

Mheshimiwa Spika, Ni vema serikali ikathamini mchango wa Mifuko ya Jamii Nchini kwa kuhakikisha kuwa haitoi dhamana ya ukopaji wa Fedha za Mifuko kwa Makampuni binafsi kwani uzoefu umeonyesha mara nyingi fedha hizo zinapotea bila kurudishwa.

Aidha ,Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iongeze juhudi katika kusajili

wanachama wapya ili kuongeza mapato yao.

Kamati inaishauri Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) kuanza mara moja jitihada za kushughulikia sheria za ukokotoaji wa mafao ili kuwa na hali ya kufanana miongoni mwa mifuko yote.

Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni yake inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati ili kuwezesha mifuko kuwa endelevu.

4.1.7 VIWANGO VYA MALIPO YA CONCESSION FEES KATIKA HIFADHI ZA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Upo upotevu mkubwa wa Mapato ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia viwango vidogo vya *Concession fees* zinazolipwa na wamiliki wa hoteli za kitalii zilizopo hifadhini. Mapato ya concession fees yanapitwa kwa kiasi kikubwa na yale yanayotokana na Upigaji wa mahema (Camping) ambapo mtu mmoja hulipa USD 50 kwa siku katika Hifadhi ya Serengeti wakati concession fees ni wastani wa USD7- 10 kwa mtu mmoja kwa siku. Malipo kama haya yameisababishia TANAPA kutopata mapato ya shilingi bilioni 19 kwa mwaka wa fedha 2008/2009. TANAPA ilikusanya jumla ya shilingi Bilioni 2.4 kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kutokana na malipo ya concession fees.

Mheshimiwa Spika, TANAPA imependekeza viwango vya concession fees vitozwe kwa kuzingatia fixed rate kwa hotel zote ili kudhibiti upotevu wa mapato hivyo Kamati inapendekeza maoni hayo ya TANAPA yaliyofikiwa kitaalamu ndiyo yatumike ili waweze kutoza kati ya dola za kimarekani 20 hadi 30 kutokana na hoteli husika kwa viwango vya fixed rate ili Taifa letu lipate thamani halisi ya rasilimali

zetu.

4.1.8 SHIRIKA HODHI LA YALIYOKUWA MASHIRIKA YA UMMA (CHC)

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Novemba mwaka 2007, Bunge lako Tukufu lilipitisha mabadiliko ya sheria namba 26 ya mwaka 2007 iliyokuwa inaanzisha Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma na badala yake ikaanzisha na kukasimisha majukumu kwa Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya umma, CHC ili itekeleze majukumu ya iliyokuwa PSRC.

Tokea kuanzishwa kwake CHC imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maslahi ya Serikali na Umma kwa ujumla yanalindwa ipasavyo katika utekekelezaji wa sera ya ubinafsishaji. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2009 CHC wamekusanya shilingi bilioni 2.6 ukilinganisha na shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2008 na pia kukusanya shilingi bilioni 14.3 kama gawiwo na kwenye Hisa mbali mbali.

Mafanikio makubwa yamepatikana ikiwamo ukusanyaji wa madeni na pia tathimini ya matokeo ya sera ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika,muda wa uhai wa CHC unafikia ukomo kisheria mwezi juni mwaka 2011, Kamati inaishauri Serikali kuiongezea CHC muda wa kutosha mapema iwezekanavyo ili ikamilishe shughuli ambazo bado hazijakamilika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa deni la serikali linalofikia Jumla ya shilingi bilioni 23,610,024,841 hadi tarehe 28/02/2011.

CHC kwa niaba ya Serikali ndiyo wenye taarifa muhimu za wadaiwa na waliobinafsishiwa mali za Umma hivyo iwapo hawatapewa muda

zaidi wa kukamilisha majukumu yao kuna hatari kubwa ya serikali na umma kwa ujumla kupata hasara kubwa kwa wadaiwa kuficha taarifa zao.

4.1.9 KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya ndege Tanzania (ATCL) inapitia kipindi kigumu cha uendeshaji kwa kukosa mtaji wa kuweza kufanikisha shughuli zake.Kampuni hii kwa sasa haina uwezo wa kurusha ndege yeyote kutokana na mzigo mkubwa wa madeni unaolikabili Shirika hili likiwa na madeni yanayofikia 23.3 bilioni na Mtaji Hasi (negative equity) wa shilingi 23.3 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri na kupendekeza kwa Serikali kuchukua madeni yote ya ATCL na baada ya hapo kutoa mtaji (unaofikia dola za kimarekani 31 bilioni) wa kuanza kuliendesha Shirika hili ikiwa ni pamoja na kutoa dola laki saba ili kuirudisha ndege ya ATCL iliyopo kwenye matengenezo ili ianze kufanya kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika,Kamati haikubaliani kabisa na kuendelea kusubiri Mwekezaji kwenye ATCL kwa zaidi ya miaka mitano sasa Shirika likiwa limesimamisha shughuli zake bila kujua hatma yake, aidha Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunda upya Bodi na Menejimenti ya ATCL ili iweze kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Shirika hilo kwa haraka na kwa ufasaha.

4.1.10 KUTOA MTAJI KWA SHIRIKA LA TIJA LA TAIFA (NIP)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa (NIP) ni chombo muhimu kinachoweza kulisaidia Taifa katika kuhakisha shughuli zinafanyika kwa Tija ikizingatiwa uchache wa rasilimali tulizonazo.shirika hili lilianzishwa mnamo mwaka 1974 likilenga kutoa mafunzo ya menejimenti, upimaji tija na kutoa huduma za ushauri na kuchangia harakati za taifa kujenga uchumi imara na maisha bora kwa kila mtanzania.

Mheshimiwa Spika, shirika hili ambalo likitumiwa vizuri litapunguza upotevu wa fedha za umma unaofanyika katika nyanja za mafunzo toka kwa taasisi ambazo baadhi hazina nyenzo na uwezo wa kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa,halipati ruzuku toka serikalini ili kujiendesha kwa ufanisi, ni ushauri wa Kamati kupitia Wizara mama ya shirika hili (Wizara ya Kazi Ajira na Vijana) kuingiza mpango kazi wa Shirika hili utakaogharimu shilingi bilioni 1.5 ili kulipa uwezo na nyenzo za kufanyia kazi ili liweze kuwa ***think tank*** ya Taifa katika maeneo ya kuongeza tija na ufanisi.

4.1.11 TATHIMINI YA MATOKEO YA UBINAFSISHAJI (POST PRIVATIZATION EVALUATION)

Mheshimiwa Spika, lengo la ubinafsishaji ni kuinua uchumi wa Taifa na watu wake. Kwa mantiki hiyo basi , Kamati inashauri Msajili wa Hazina aweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji walioshindwa kutekeleza masharti ya uwekezaji.

Aidha pia Kamati inapendekeza kwa Serikali kuchukua uamuzi wa kurudisha chini yake umiliki wa baadhi ya mali zilizouzwa kwa wawekezaji na baada ya hapo zimetelekezwa au matumizi

yaliyoainishwa kwenye mikataba ya ununuzi yamekiukwa.

4.1.12 KUANZISHWA KWA MFUKO MAALUM WA UWEKEZAJI (SPECIAL INVESTMENT FUND)

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Umma yalianzishwa kwa makusudi makubwa ya kutoa huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kwa muda mrefu yamekuwa yakifanya hivyo japo yanakabiliwa changamoto kubwa. Kama tulivyoeleza hapo awali changamoto kubwa ni mitaji ya kujiendesha ipasavyo.

Baadhi ya Mashirika yamekuwa yakizalisha ziada kutokana na huduma wanazotoa, mashirika haya ni kama mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Bandari Tanzania,EWURA, TCRA, SUMATRA NK.

Mheshimiwa Spika,Kamati inaafikiana na ushauri uliotolewa na CAG wa kuanzisha mfuko maalumu wa uwekezaji (special investment fund) ili mashirika yanayozalisha ziada yawekeze fedha hizo katika mfuko maalum ambao utatumika kwaajili ya kusaidia mashirika yasiokuwa na mitaji katika kuwekeza ili kusaidia kufanikisha mchango wa Mashirika ya Umma kwa maendeleo ya Taifa.

4.1.13 ENDOWMENT FUNDS ZA MASHIRIKA YA UMMA ZISIMAMIWE NA INDEPENDENT FUND MANAGERS

Mheshimiwa Spika, Mashirika mbali mbali ya umma yanatumia mfumo wa endowment scheme kama moja ya njia ya kutoa motisha kwa wafanyikazi wao na kuongeza ufanisi wa Shirika pindi watakapostaafu.Kamati ilibaini mapungufu katika uendeshaji wa mifuko hiyo ya wafanyakazi hasa ilipobainika kuwa shirika husika

ndilo pia linaendesha mfuko wa endowment.

kwa maoni ya Kamati, utaratibu kama huu sio unaokubalika kwa Sheria za Fedha, hivyo kamati inashauri Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini(SSRA) kuhakikisha kuwa Mashirika yote yenye mfuko wa endowment (mfano TANAPA na NSSF) wanaanza mchakato wa kutenganisha endowment funds ili ziwe chini ya uangalizi wa Independent Fund Managers (best practice on finincial management)

4.1.14 MIRADI YA MCHUCHUMA, LIGANGA NA KIWIRA

Mheshimiwa Spika, baada ya ziara ya Kamati kukagua miradi ya Mchuchuma, Liganga na Kiwira inayoendeshwa chini ya usimamizi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na ule wa Kiwira ambapo Kamati ilifuatilia utekelezwaji wa sera ya ubinafsishaji naomba kuwasilisha Mapendekezo na Maoni ya Kamati juu ya miradi hiyo muhimu kwa Taifa letu,

1. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inalipongeza Shirika la NDC kwa hatua kubwa waliofikia katika Miradi ya Mchuchuma, Liganga na South Ngaka. Hata hivyo juhudi zaidi zinatakiwa ili kuhakikisha kuwa miradi hii inatekelezwa katika muda mwafaka.

2. **Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Ubia baina ya Shirika la NDC na Kampuni Sichuan Hongda toka China ili kuendeleza Mradi wa Mchuchuma-Liganga ni muhimu usainiwe sasa na haraka na Serikali ishauriwe kutimiza wajibu wake kwa hatua ambayo NDC imefikia ikizingatiwa Faida za kiuchumi za Mradi huu. Mazingira ya sasa ya uchumi wa Dunia na mahitaji ya Taifa ni mwafaka kwa miradi ya Makaa na Chuma. Kuchelewa kuanza kwa miradi hii kwaweza sababisha miradi isifanyike kabisa kwani uchumi wa dunia kwenye bidhaa za chuma huwa unayumbayumba sana (fluctuations).

3. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni tanzu itakayoundwa ili kuendesha miradi hii ifuate taratibu zote za uchimbaji ikiwemo kusainiwa kwa Mkataba wa Uendelezaji Migodi (Mineral Development Agreements-MDA) kwa madhumuni ya kulinda maslahi ya Serikali, Watu wa Ludewa na Kampuni yenyewe.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa suala la Ubia bado halijaamuliwa, Kamati inashauri kuwa ubia uzingatie kanuni ya Faida (profitability and Pay Back period). Kwa mfano, NDC waweza kuanza kwa kuwa na hisa 20% lakini mara baada ya mradi kulipa (payback period) mgawo wa hisa uwe ni sawa kwa sawa. Pendekezo hili pia lizingatiwe kwa mradi wa Ngaka ambapo NDC wanahisa 30% kwenye Kampuni tanzu ya TANCOAL Energy.

5. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nishati na Madini iharakishe kutoa leseni ya uchimbaji wa Makaa ya Mawe kama ilivyoombwa na Kampuni ya TANCOAL ambayo inamilikiwa kwa ubia na NDC ili uchimbaji wa makaa uanze na hivyo kuanza kuzalisha Umeme. Inapendekezwa kuwa Umeme unaotokana na Makaa ya South Ngaka uzalishwe kutokea Wilaya ya Kyela ili kurahisisha kuunganisha na gridi ya Taifa.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwa Kamati ya Nishati na Madini kuanza mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini kwa lengo la kutangaza kwamba Rasilimali za Makaa ya Mawe na Chuma kuwa ni Rasilimali za kimkakati (strategic resources) na kwamba leseni za kumiliki vitalu vya Madini haya zitamilikiwa na Mashirika ya Umma tu. Pendekezo hili linatokana na ukweli kwamba kuna leseni nyingi sana za kumiliki Madini haya ambazo zimemilikishwa kwa watu binafsi (speculators). Inapendekezwa kwamba leseni zote za kumiliki vitalu vya Chuma na Makaa ya Mawe zinazomilikiwa na watu binafsi au Makampuni ya nje **zifutwe** na kumilikishwa kwa ama STAMICO au NDC. Hata hivyo, ifikiriwe kuundwa kwa Shirika la TANZANIA IRON AND COAL CORPORATION itakayomilikiwa kwa ubia na STAMICO na NDC na Shirika lingine lolote la Umma kwa lengo la kuendeleza rasilimali ya Makaa ya Mawe na Chuma hapa Nchini.

7. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inalitaka Shirika la Umeme Nchini TANESCO kuanza kuwekeza katika msongo wa kusafirisha Umeme

(TRANSMISSION) kuelekea kwenye miradi hii ili kufanya miradi hii iwe na maana. Kamati imefurahishwa na wazo la wabia wa NDC kujenga msongo wao wa umeme. Hata hivyo, Kamati inaamini kuwa suala la msongo wa umeme liendelee kuwa chini ya Shirika la TANESCO au Serikali iunde Kampuni nyingine ya Umma kwa ajili ya Transmission peke yake. Kwa ajili ya uharaka wa msongo wa sasa Kamati inashauri kuwa wabia wa NDC wajenge msongo huu kama mkopo kwa Shirika la TANESCO.

4.1.15 MASHIRIKA YA UMMA KUZINGATIA MASLAHI YA TAIFA WAKATI WA KUFANYA MANUNUZI

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa manunuzi yote yanayofanywa na Mashirika ya Umma, Aidha ni vema ikafahamika kuwa miongoni mwa Mashirika yote ya Umma hapa Nchini ni TANESCO ndio wanaofanya manunuzi ya gharama kubwa kwa mwaka ukilinganisha na Mashirika mengine hivyo basi Kamati inashauri kuwa **p**ale ambapo Serikali ina hisa katika Kampuni ambayo inazalisha hapa hapa Nchini baadhi ya bidhaa zinazohitajika na Mashirika ya Umma basi, Mashirika ya umma yatoe kipaumbele cha manunuzi yao bila kuathiri ubora. Kwa mfano haiingii akilini Shirika la Umeme Tanzania kununua nyaya kutoka nje wakati Serikali inamiliki hisa katika East African Cables ama kununua transforma kutoka nje wakati Serikali ina hisa tanelec. Kisingizio ni sheria ya Manunuzi, Sheria gani inayotoa fursa za kukuza Viwanda vya nje na kunyima Kazi na hivyo ajira kwa Viwanda vya ndani? Kamati inapendekeza kwamba Mashirika ya Umma yaingie mikataba ya muda mrefu (supply contracts) na Viwanda vya ndani vyenye kuzalisha bidhaa wanazotumia ili kuimarisha Viwanda

vya ndani na Pendekezo hili lianze kwa TANESCO kuhusiana na trasnforma na nyaya

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, ninayofuraha kwamba Taarifa ya Kamati imeeleza namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake ya msingi na mafanikio iliyopata katika utekelezaji wa majukumu yake hivyo kuridhihirishia Bunge lako umuhimu wa Kamati hii katika kusimamia ufanisi wa mashirika ya umma nchini.

Hivyo Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kwa jinsi tulivoshirikiana katika kuweka mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa Bunge na Kamati zake hususani Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeniwezesha mimi kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni, umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mhe. Deo Haule Filikunjombe, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana kwa uadilifu wao, michango na hoja zao zilizolenga maslahi ya Taifa kwa muda wote. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto, MB - Mwenyekiti
2. Mhe. Deo H. Filikunjombe, MB - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Felista Aloyce Bura, MB - Mjumbe
4. Mhe. Juma Abdallah Njwayo, MB - Mjumbe
5. Mhe. Alphaxard Kangi Ndege Lugola, MB - Mjumbe
6. Mhe. Muhamad A. Chomboh, MB - Mjumbe
7. Mhe. Murtaza Ally Mangungu , MB - Mjumbe
8. Mhe. Aliko Nikusuma Kibona, MB - Mjumbe
9. Mhe. Jerome D. Bwanausi, MB - Mjumbe
10. Mhe. Ali Kheir Khamis, MB - Mjumbe
11. Mhe. Prudensiana W. Kikwembe, MB - Mjumbe
12. Mhe. Esther N. Matiko, MB - Mjumbe
13. Mhe. Christowaja G. Mtinda, MB - Mjumbe
14. Mhe. Zainab Rashid Kawawa, MB - Mjumbe
15. Mhe. Amina Mohamed Mwidau, MB - Mjumbe
16. Mhe. Ester Amos Bulaya, MB - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Shukrani zaidi kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuendelea kuipangia Kamati Katibu makini na ambaye ameratibu na kuishauri Kamati kwa ufasaha juu ya mwenendo bora wa shughuli za kila siku kwa kuzingatia miongozo ya utendaji kazi za Bunge na Kamati zake kwa muda wote , Huyu ni Ndugu. Erick Maseke.

Naomba kutumia fursa hii kuishukuru Benki ya Dunia kwa programu yake ya Urekebeshij wa Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma inayojulikana kama (public finincial management reform programme) kwa kifupi kama PFMRP kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza ziara mbalimbali za kukagua ufanisi wa mashirika.

Nawashukuru pia Maafisa wote kutoka Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kurekodi mijadala mbalimbali ya Kamati na kwa kuchapa taarifa hii. Shukrani pia kwa Maafisa wa Polisi kutoka kitengo cha Ulinzi cha Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Usalama katika Ziara zote tulizo ambatana nao. Nawashukuru Watumishi wote wa Bunge walioisaidia Kamati kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nawashukuru Wataalam kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali (CAG), Ofisi ya Msajili wa Hazina(TR) na Maafisa kutoka Shirika Hodhi linaloshughulikia Madeni na Mali ya yaliyokuwa Mashirika ya umma (CHC) kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza majukumu yake vema.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Wakurugenzi mbalimbali wa Mashirika ya Umma nchini kwa utayari wao kila walipotakiwa kutoa maelezo, elimu na ufafanuzi wa aina mbalimbali kila walipohitajika kufanya hivyo mbe le ya Kamati.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza .

Naomba kutoa Hoja.

Mhe. Kabwe Z. Zitto, Mb.
MWENYEKITI
KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA
APRIL, 2011



Wajumbe wa Kamati ya POAC walipofanya Ziara ya ukaguzi wa miradi ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) Mradi wa chuma (Liganga) kama unavyoonekana wilaya ya Ludewa Mkoa mpya wa Njombe tarehe 08 Machi, 2011